Wilaya ya Arumeru kujenga uwanja wa kisasa

"Tayari nimeishapata wadhamini wa kusaidia mpango wa kukuza soka kwa vijana, tutapeleka vijana 20 Brazil lil wakirudi wawe mfano nchini."

Nyerembe Munasa, Mkuu wa Wilaya.

Happy Lazaro, Mwananchi

Arusha. Wilaya ya Arumeru ipo mbioni kujenga uwanja mkubwa wa kisasa wa soka katika Halmashauri ya Meru ikiwa ni mpango wa kuendeleza michezo katika Wilaya hiyo kwani wana timu nyingi za vijana.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya hiyo, Nyerembe Munasa wakati akizungumza katika hafla ya utoaji zawadi kwa mabingwa wa ligi maalumu iliyoanzishwa kwa ajili ya timu za vijana Wilayani Arumeru mkoani Arusha na mdau wa michezo kutoka Ufaransa, Damian Sellier katika mji mdogo wa Usa River eneo la Leganga.

Munasa alisema kuwa hiyo ni mikakati yake katika kukuza michezo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Meru, ambapo tayari eneo la ujenzi huo limeshapatikana na kinachofuata ni mipango ya ukusanyaji fedha kwa ajili ya ujenzi huo kuanza.

Alisema kuwa kabla ya ujenzi wa uwanja huo kukamilika wanatarajia kuanzisha mashindano ya vijana wadogo kutafuta vijana 20 bora ambao watakuwa waanzilishi wa timu maalumu ya Wilaya hiyo ambayo mwakani itapelekwa Brazil kwa ajili ya mafunzo maalumu.

"Tayari nimeishapata baadhi ya wadhamini kusaidia mpango wa kukuza soka kwa vijana na tumekubaliana kuanza na vijana 20 ambao watapelekwa Brazil kwa ajili ya mafunzo maalumu ili wakirudi wawe ndiyo mfano kwa soka la nchi hii," alisema Munasa.

Alisema vijana hao ambao watatumia uwanja huo ndiyo watakuwa wa kwanza kutumia uwanja huo wa kisasa kama uwanja wa nyumbani na kuvutia timu nyingi kufika katika wilaya hiyo kwa ajili ya kutumia uwanja huo.

Naye Mratibu wa kituo cha Usa River Youth ambao ndiyo walikuwa wasimamizi wa ligi hiyo, Daudi Mkumba alimshukuru mkuu wa wilaya na mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru kwa ushirikiano wao ila aliwaomba pia kuhakikisha wanatoa ushirikiano zaidi kwa taasisi zinazoanzisha mashindano ya vijana ili kukuza na kuibua vipaji vya vijana.

Alisema Serikali ikisaidia zaidi michezo, kituo cha Usa River Youth kitakuwa katika nafasi nzuri ya kutoa motisha ya zawadi kwa vijana wanaofanya vizuri tofauti na ilivyo sasa.

SOKA

Morocco: Yanga, Simba hazinitishi, naihofia Azam

Kocha wa Coastal Union, Hemed Morocco anaamini Azam ndiyo timu ambayo imejipanga kwa kila kitu na kukaa pamoja.

Calvin Kiwia, Mwananchi

Dar es Salaam. Kocha Mkuu wa Coastal Union, Hemed Morocco ameweka wazi kuwa Yanga na Simba hazimpi presha ingawa amekiri Azam FC ndiyo timu inayokatisha usingizi wake.

Akizungumza na gazeti hili katika mahojiano maalumu mjini Tanga, kocha huyo wa zamani wa Zanzibar Heroes alisema, "Yanga na Simba hazinitishi kabisa, wala siwezi kuumiza kichwa kuzifikiria kabla ya kukutana nao kwenye ligi msimu huu, ni timu za kawaida sana kwangu, najua jinsi ya kuwakamata."

Alisema, "nafikiri Azam ndiyo timu tishio kwenye ligi msimu huu tofauti na Simba na Yanga."

Morocco ambaye amepania kutwaa taji la ubingwa wa ligi msimu huu au kupata nafasi ya kuiwakilisha nchi katika michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF) alisema kuwa Azam ni timu pekee ambayo imefanya maandalizi ya nguvu zaidi kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa ligi na wachezaji wake wamekaa kwa kipindi kirefu pamoja bila kusahau kukamata mara mbili mfululizo nafasi ya pili.

"Unajua ukikutana na Azam, lazima utulize akili yako vizuri, ni timu ambayo imejipanga kwa kila kitu na kukaa pamoja tofauti na Simba na Yanga wanaocheza soka lao kwenye vyombo vya habari," alisema Morocco.

"Azam kupoteza michezo miwili kati ya mitatu ya kirafiki kule Afrika Kusini na ule wa Ngao ya Jamii juzi dhidi ya Yanga, siyo tatizo, ni sehemu ya mwalimu kufanya masahihisho," alisema kocha Morocco.

Azam iliweka kambi yake Afrika Kusini siku 10 na kucheza mechi tatu na kushinda moja dhidi ya Mamelodi Sundowns kwa bao 1-0, kabla ya kupoteza dhidi ya Orlando Pirates 2-1 na Kaizer Chiefs 3-0.

WANAUME: HAPA KAZI

Wanamuziki wa kutoka TMK Family, Chege (kulia) na Temba (kushoto) wakitumbuiza katika tamasha la Serengeti Fiesta mjini Kigoma kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika. Picha na Mpigapicha Wetu.

BWANA CHEZO Na Ibra Washokera

Spoti Dondoo

Tanzania, Msumbiji kukipiga Afrika

Dar es Salaam. Timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania chini ya miaka 20 imepangwa kuanza moja kwa moja raundi ya kwanza Kanda ya Afrika kutafuta tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia za Wanawake zitakazofanyika mwakani nchini Canada.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa juzi Agosti 18 na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Tanzania imepangiwa kucheza na Msumbiji.

Mechi ya kwanza itachezwa jijini Dar es Salaam kati ya Oktoba 25, 26 au 27 na ile ya marudiano itachezwa wiki mbili baadaye nchini Msumbiji kati ya Novemba 8, 9 au 10 mwaka huu.

Tanzania iwapo itafanikiwa kuitoa Msumbiji itacheza raundi ya pili na mshindi wa mechi kati ya Botswana na Afrika Kusini. *(Sweetbert Lukonge).*

Ashinda gari katika tamasha la Fiesta

Dar es Salaam. Mkazi wa Kigoma, Abdallah Ally Ngagari (51) ameshinda gari aina ya Vitz kwenye bahati nasibu iliyoendeshwa na kampuni ya Push Mobile Media ya kunogesha tamasha la Fiesta.

Meneja Masoko na Mauzo wa Push Mobile Media, Rugambo Rodney alisema kuwa tayari Ngagari amekabidhiwa gari lake huko Kigoma.

Rugambo alisema kuwa baada ya kukamilisha bahati nasibu hiyo, kwa sasa nguvu zao wanazielekeza mkoani Tabora katika tamasha la Fiesta ambalo litafanyika Ijumaa.

Alisema kuwa watatoa pikipiki kwa wapenzi wa muziki wa Tabora, ambapo ili kushinda, mashabiki wanatakiwa kutuma neno Fiesta kwenda namba 15678 ili kushinda pikipiki au fedha taslimu sh 100,000. *(Imani Makongoro).*

Javu afurahia medali

Dar es Salaam. Mshambuliaji mpya wa Yanga aliyejiunga na klabu hiyo akitokea Mtibwa Sugar, Hussein Javu, juzi Jumamosi alishangilia kuvaa medali kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka.

Javu alishangilia hali hiyo baada ya Yanga kufanikiwa kuitandika Azam FC bao 1-0 katika mchezo wa kuwania Ngao ya Jamii uliofanyika kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam na kutwaa ngao hiyo huku wachezaji na viongozi wa benchi la ufundi wakizawadiwa medali kila mmoja.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Javu alisema kuwa anajiona ni mwenye bahati kubwa kujiunga na Yanga kwani kwa muda mfupi tu ameweza kuandika historia katika maisha yake ya soka kwa kuvaa medali. *(Sweetbert Lukonge).*